**CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO**
NAMBA YA USAJILI 5596,
S.L.P 140 LINDI
Email:lindimwambaocoopunion@yahoo.com

# TANGAZO LA ZABUNI YA USAFIRISHAJI UFUTA NA MBAAZI MSIMU - 2026

**LMCU/LD/HQ/2026-2027/NC/ 01**

**09/04/2026.**

MWENYEKITI WA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO LTD ANAWATANGAZIA MAKAMPUNI AU WENYE MAJINA YA BIASHARA WILAYA YA KILWA, HALMASHAURI YA MTAMA NA LINDI MANISPAA KUOMBA ZABUNI YA KUSAFIRISHA UFUTA NA MBAAZI KUTOKA KWENYE VYAMA VYA MSINGI NA KUFIKISHA KWENYE MAGHALA YA MNADA YALIYOPANGWA CHINI YA MFUMO WA STAKABADHI MAZAO GHALANI.

**SIFA ZA WAOMBAJI.**

1. Mwombaji aambatanishe nakala ya Leseni hai ya biashara(Active business licenses)inayohusiana na usafirishaji wa mazao.

2. Mwombaji aambatanishe nakala ya namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN Number)
3. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax Clearance Certificate)
4. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya zabuni Tshs. **500,000/= (Laki Tano tu) "Hairudishwi"** katika akaunti namba **0150267283200 (LINDI MWAMBAO COOPERATIVE UNION-LTD) CRDB BANK,** na aambatanishe risiti pamoja na barua ya maombi yaliyofungwa katika bahasha kwa lakili.
5. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha uthibitisho wa mmiliki mwenye nguvu ya kisheria ( POWER OF ATTORNEY)
6. Mwombaji aambatanishe taarifa za kibenki ya mwaka mmoja(1) kuanzia $01^{st}$ January 2025- $9^{th}$ April 2026 .

7. Mwombaji awasilishe taarifa za fedha za miaka miwili (2) Financial statements, ya hivi karibuni.

8. Mwombaji awe Kampuni/ Jina la biashara(Iliyosajiliwa na BRELA)
9. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka miwili ya kufanya kazi ya usafirishaji wa mazao.(Kiambatisho ni mikataba mitatu ya kazi za usafirishaji ya karibuni)
10. Mwombaji aambatanishe nakala za kadi za gari zisizopungua kumi zenye uwezo wa kubeba tani (15) au (30) kwa kila gari moja, zitakazotumika katika shughuli za usafirishaji ,na kama si mmiliki halali aambatanishe Pamoja na mkataba halisi wa kukodi gari husika unaotambulika na mwanasheria.
11. Mwombaji atapaswa kujisajili na kulipa ada ya mwaka tume ya maendeleo ya ushirika TCDC na kuambatisha cheti cha usajili wa mtoa huduma kwa vyama vya ushirika **2026**.
12. Mwombaji atakayeshinda zabuni anatakiwa kulipa fedha ya kinga ya dhamana Tshs. ***5,000,000/=*** **(Milioni Tano tu)** kabla ya kusaini mkataba,ambazo mwisho wa msimu atarudishiwa endapo hatasababisha hasara yoyote kwenye Chama. Fedha hizo zilipwe katika akaunti namba **0150267283200- LINDI MWAMBAO COOP UNION LTD ndani ya masaa 72 baada ya kupata barua ya ushindi wa zabuni.**
13. Mwombaji atapaswa kuaandaa kitabu kilichoambatishwa vielelezo vilivyoainishwa na kuwasilisha kwa katibu bodi ya zabuni Lindi Mwambao-LTD.
14. Tangazo hili litadumu kwa muda wa siku **14** kuanzia **09 April 2026 - 22 April 2026.**
15. Maombi yote yafungwe kwa lakiri na yatumwe kwa **KATIBU BODI YA ZABUNI CHAMA KIKUU CHA USHIRIKIA LINDI MWAMBAO-LTD** na kuwasilishwa katika ofisi ya Chama Kikuu Lindi Mwambao iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa Lindi -Mitwero. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **22/04/2026** saa 10:00 jioni

MENEJA MKUU,
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO,
S.L.P. 140,
**LINDI.**

LINDI MWAMBAO COOP UNION LTD
GENERAL MANAGER
AFF-LND-LND-MC-2023-24
P.O.Box 140, LINDI